**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

**WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI**

Dar es Salaam-20 Machi, 2025

# TAARIFA KWA UMMA

## UWASILISHAJI WA TAARIFA WA UMILIKI WA FAIDA KATIKA KAMPUNI

Taarifa inatolewa kuhusu takwa la kampuni zote za Kitanzania kuwasilisha taarifa za wamiliki wa mwisho wa manufaa katika kampuni ambalo ni takwa la kisheria chini ya Kifungu cha 459A cha Sheria ya Makampuni, Sura ya 212 na Kanuni za Umiliki wa Manufaa za mwaka 2023, zilizochapishwa kupitia Tangazo la Serikali Namba 714 ya tarehe 22 Septemba, 2023.

Kwa muktadha huu, Msajili anautangazia umma kwamba kuanzia tarehe 15 Februari, 2025, kampuni yoyote ya Kitanzania ambayo haijawasilisha taarifa za wamiliki manufaa wake haitaweza kufanya muamala wowote na Msajili hadi hapo itakapowasilisha taarifa hizo. Miamala itakayozuiliwa ni; uwasilishaji wa marejesho ya mwaka, mabadiliko mbalimbali kwenye kampuni, maombi ya taarifa za hali ya kampuni, usajili wa dhamana, upekuzi, maombi ya kuingia kwenye mfumo kwa waliopoteza uwezo wa kuingia, na uidhinishaji nakala za nyaraka halisi.

Ifahamike kwamba Msajili alitoa muda wa kutosha wa kuwasilisha taarifa hizo tangu mwezi Juni 2022, hata hivyo hadi sasa kuna kampuni ambazo hazijafanya hivyo.

Uwasilishaji wa taarifa hizi unafanyika kupitia mfumo wa kieletroniki na maelezo ya jinsi ya kujisajili yanapatikana katika anuani https://bo.brela.go.tz.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na BRELA kupitia baruapepe usajili@brela.go.tz au piga simu namba 0222212800.

Imetolewa na;
**Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma**